**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OWM - TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE.**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAGERA RIVER,**
**S. L. P. 452, KARAGWE**

**SIMU: Mkuu wa shule 0756317322/0773317322, Makamu 0753157662/0657167662, Mtaaluma 0758160125, Nidhamu 0783680425.**
**Gmail.** kagerarivergirls2024@gmail.com
**Inakopatikana kwenye ramani:** https://maps.app.goo.gl/ptEX3mgVhtDUtRij8

Jina sahihi la mwanafunzi: ______________________________________________
Tahasusi (Combination) aliyochaguliwa ______________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAGERA RIVER WILAYA YA KARAGWE MKOA WA KAGERA MWAKA............**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha **tano,** katika shule hii mwaka.......... **Shule ya Sekondari ya Wasichana Kagera river** ipo kusini mwa kituo cha mabasi cha Kayanga, kilichopo Mji mdogo wa Kayanga wilaya ya Karagwe. Ukifika Bukoba mjini mkoa wa Kagera, tafuta magari yanayoelekea Karagwe na ushuke stendi ya Kayanga (nauli ni sh. 5,000 safari ya masaa mawili). Ukifika stendi ya Kayanga tafuta magari yanayoenda Rwambaizi (nauli ni sh 4,000 safari ya dakika 40). Ukifika Rwambaizi taja jina la shule Kagera river sekondari utapelekwa shuleni kwa pikipiki (nauli ni sh. 2000 safari ya dakika tano).

**Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe...............**

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti kuanzia tarehe....................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe................

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

**1. Sare ya shule**

- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo:-**

(i) Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu aina ya Halua

(ii) Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni sidiria au vesti ziwe za rangi nyeupe haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na nyeupe ndani ya shati la shule.

(iii) Sketi mbili (2) rangi ya **Idara ya maji dark** kitambaa cha suti orginal ndefu mpaka kwenye kisigino**.**

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi Jozi 2 vyenye kamba, visigino vifupi na Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote.

(v) Buti nyeusi pea moja kwa ajili ya kuvaa wakati wa mvua kubwa

(vi) Jozi tano za soksi nyeupe zisizo na mistari (stocking) zinazofika magotini.

(vii) Wanafunzi wa Kiislamu, **(Juba)** nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua, zisizo na urembo wa aina yoyote na juba mbili za **dark blue** ndefu kwa ajili ya kushindia.

(viii) Tai rangi ya blue yenye michilizi nyeupe na nembo ya shule.

(ix) Masweta mawili yenye nembo ya shule rangi ya **dark blue**.

(x) Tisheti yenye kola na nembo ya shule nzito rangi ya **dark blue** isiyo changanyikana na rangi nyingine (isiwe ile yenye mistri kwenye kola) iwe rangi moja tu.

(xi) Shamba dress (Gauni mbili ndefu za rangi ya **kijani** mshono wa solo kitambaa kizito cha suti kwa ajili ya kushindia na kazi za nje)

(xii) Traki suti ya rangi ya **dark blue** (yaani suruali, tisheti na sweta) isiyokuwa na maandishi.

(xiii) Koti kubwa na zito jeusi kwa ajili ya kujikinga na baridi hasa wakati wa usiku.

(xiv) **Kwa ajili ya michezo:** Tisheti nyekundu isiokuwa na kola, Sketi fupi nyekundu isiyovuka magoti, na skini ndefu nyeusi na raba nyeupe pamoja na tisheti ya rangi nyeupe na bukta yake.

(xv) Mwanafunzi wa PCB aje na dissection kit (box)

(xvi) Kwa mwanafunzi asiye na kadi ya Bima ya Afya aje na kiasi cha Tsh 50,400 kwa ajili ya kukatiwa Bima ya afya.

***ZINGATIA:***

***N.B: Ili kuepuka kukosea rangi ya kitambaa cha sketi ni vizuri Mzazi/Mlezi ufike karibu na maeneo ya shule kwa ajili ya kijiridhisha.***

***(i) Nguo zote ziwekewe alama ya utambuzi ili kudhibiti wizi (alama yoyote ya kumsaidia mhusika kutambua kuwa ni ya kwake)***

***(ii) Ili kuepuka changamoto ya kukosea rangi, aina ya sare sketi,Tisheti,sweta na***

KAGERA RIVER GIRLS SECONDARY SCHOOL EDUCATION FOR LIBERATION

***Tai zinapatikana maeneo yaliyo karibu na shule lakini kwa watakao hitaji.***

**2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa na cheti cha kidato cha nne (Ni lazima kwa kila mwanafunnzi)

ii. Madaftari 12 aina ya counter books quires 3 na box file mbili.

iii. **Ream mbili (A4)** za karatasi (Aina ya **A-one** au **DoubleA** zinapendekezwa zaidi)

iv. Vitabu vya mtaala mpya kwa masomo ya tahasusi uliyochaguliwa kati ya PCB, PCM, EGM, HGK na HGL.

v. Godoro lenye vipimo vya 2.5X6 (Kwa mwenye matatizo ya kukojoa kitandani godoro lake lifunikwe kwa mpira wa kuzuia mkojo)

vi. Mashuka Jozi 3 za rangi ya pinki, blanket 1, foronya 1 lenye foronya ya rangi ya pink, chandarua 1 yenye rangi nyeupe.

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani ya chuma yenye vijisehemu vitatu, kijiko na kikombe cha chuma).

ix. Ndoo 2 kubwa za lita 20 zenye mifuniko, beseni moja na kidumu cha lita tano cha kutunzia maji ya kunywa.

x. Toilet papers tano kubwa.

**xi. Vifaa vifuatavyo viletwe kwa michepuo kama ifuatavyo:**

a)PCB walete kotama na jembe

b) PCM walete kotama na jembe la meno

c)EGM walete kotama kwanja na leki,

d) HGL, HKL na HGK walete kotama na jembe

x. Sanduku la mbao au chuma na kufuli lake kwa ajili ya kutunza vitu bwenini.

xi. Aje na vifaa vya usafi binafsi kama: Sabuni, mafuta ya kujipaka, mswaki, dawa ya meno, dawa ya viatu, brashi na kandambili.

xii. Tochi inayotumia mwanga wa jua/betri (isiyochajiwa kwa umeme).

xiii. Scientific calculator moja toleo la kisasa (fx 991) kwa wanafunzi wa michepuo ya sayansi. (Sokoni kuna tatizo kubwa la kuwa na calculator feki. Kama hauna uzoefu wasiliana nasi.

xiv. Picha 4 passport size akiwa amevaa shati la shule (jeupe) na ziwe na kivuli cha bluu nyuma. Picha hizi zifungwe vizuri kwenye kipande cha karatasi na kubanwa na stapler juu kushoto mwa fomu hii.

xv. Taulo, kitenge au kanga doti moja atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

xvi. Viatu vya wazi (open shoes) kwa ajili ya kushindia.

xvii. Kila mwanafunzi aje na vifaa muhimu vya usafi vifuatavyo: mifagio 1 wa ndani (soft bloom (PCB&PCM) hard broom (EGM)), ufagio mmoja wa nje aina ya chelewa, squizer au mopper.

KAGERA RIVER GIRLS SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

## 2.2. Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000.00 |
| 2 | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3. | Nembo | 5,000.00 |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000.00 |
| | **Jumla** | **80,000.00** |

**N.B Malipo yatakayolipwa benki ni ya kipengele 2.2 tu na yalipwe kwenye akaunti ya shule benki ya CRDB namba 0150849012800 jina la akaunti SHULE YA WASICHANA KAGERA.**

**KUMBUKA:**

***Simu haziruhusiwi shuleni, hivyo kwa namna yoyote ile mwanafunzi asije na simu shuleni au kifaa chochote kinachohusiana na simu.**

*** Mwanafunzi analazimika kuvaa sare za shule wakati wote awapo shuleni, Hivyo asije na nguo za nyumbani bali aje akiwa amevaa shamba dress au tracksuit.**

KAGERA RIVER GIRLS SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

**KIAMBATISHO A.**

**3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekinolojia, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi hapa chini na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mwnafunzi akimwona mtu mzima ni sharti asimame na kumsalimia na endapo ana mzigo ampokee.

(c) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(d) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya asubuhi na jioni (Preparation).

(e) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(g) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(i) Mwanafunzi atalazimika kuzingatia ratiba ya shule wakati wote awapo shuleni.

(j) Kutunza mali za shule na kuzilinda ni jambo la lazima.

(k) Mwanafunzi atalazimika kuhudhuria vipindi vyote vya dini kwa mujibu wa ratiba ya shule.

**TANBIHI**

Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika Bwalo au mazingira yoyote ndani na nje ya shule, isipokuwa bafuni wakati wa kuoga na bwenini.

Wageni wa mwanafunzi wanaotambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka).

- Mzazi unatakiwa kuandaa pesa ya nauli ya kuja likizo fupi (kipindi cha likizo fupi) na likizo ndefu, mwezi Juni na Desemba na kuituma shuleni pindi tu itakapohitajika (utajulishwa ni lini utume nauli).
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na urembo wa aina yoyote kama vile hereni, bangili, mkufu na pete za aina yoyote ile shuleni.
- Shuleni haturuhusu nywele ndefu wala kusuka. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuja na nywele fupi
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa, akishindwa kuzingatia atafukuzwa shule.

KAGERA RIVER GIRLS SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

## KIAMBATISHO B.

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:**

1. Wizi.
2. Uasherati.
3. Usagaji.
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
9. Kuolewa ama kuwekwa kimada.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea, kuongoza, au kushiriki migomo na kuvuruga amani na usalama wa shule na usalama wa watu wengine.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kutoroka shuleni mchana au usiku.
14. Kuwa na simu ya mkononi shuleni au kumiliki kifaa chochote kinachohusiana na simu (line, earphone, charger n.k).
15. Kuhama bweni alipopangiwa na kulala bweni jingine bila ruhusa.
16. Kuhamisha taa ya umeme (bulb) kutoka eneo moja kwenda kupachika eneo jingine.
17. Kubadili dini awapo shuleni tofauti na aliyoandika wakati wa kuripoti shuleni.

**Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukabidhiwa shuleni na mwanafunzi pindi tu anaporipoti.**

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Muhimu:- Tafadhali njoo na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.**

HEADMISTRESS
KAGERA RIVER GIRLS SEC. SCHOOL
10 APR 2024
P.O. Box 452
KARAGWE

**Jina la Mkuu wa Shule.......................**

**Saini.................................**

**Mkuu wa shule**

KAGERA RIVER GIRLS SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

**KIAMBATISHO: C.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PREME MINISTERS OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form Five students.

Student’s full Name ______________________________________________

Age/Years _______

Blood found (red and White) ______________________________________

Stool examination _______________________________________________

Urinalysis: ______________________________________________________

Venereal Diseases test: ____________________________________________

T.B.test: ________________________________________________________

EyeTest: ________________________________________________________

Ears: ___________________________________________________________

Chest: __________________________________________________________

Spleen: _________________________________________________________

Abdomen: _______________________________________________________

Urine for Pregnant: _______________________________________________

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment (s) e.g. arm, leg etc. Infection chronic or family disease etc.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

________________________

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:_______________

KAGERA RIVER GIRLS
SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

Designation: ________________________________________________

Station: ______________________________

Date:______________________

Official Stamp:

KAGERA RIVER GIRLS
SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

**KIAMBATISHO D**

## TAARIFA ZAIDI ZA MZAZI NA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI: ____________________________________________

2. TAREHE YA KUZALIWA: ____________________

3. AMEZALIWA MKOA WA: _______________________ WILAYA: ______________

4. KABILA: _______________________________

5. DINI: _________________________ DHEHEBU: ____________________

6. JINA LA MZAZI/MLEZI ______________________________________________

7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI

MKOA: _________________________ WILAYA: ________________________

TARAFA: ________________________KATA: __________________________

KIJIJI/MTAA: _____________________ SIMU: ___________________, __________________

8. KAZI YA BABA/MLEZI__________________________________

9. KAZI YA MAMA______________________________________

10. Majina ya Ndugu wa mwanafunzi (wazazi/walezi na ndugu mmoja wa karibu na Familia) Weka picha ya ndugu husika kwenye kiboksi kilichopo mbele ya jina lake.

(a) Ndugu (1) (Baba au mlezi mkuu) JINA: __________________________________________

Uhusiano na Mwanafunzi: ______________________________________

Simu: _______________________________

(b) Ndugu Na 02 (Mama mzazi) JINA: ____________________________________________

Simu: _______________________________

(c) Ndugu Na 03(Ndugu mwingine) JINA: _________________________________________

Uhusiano na Mwanafunzi_________________________________________________

Simu______________________________

……………………………………
**SAINI YA MWANAFUNZI (Isiwe ya kukoroga)**

TAREHE:………………………..

KAGERA RIVER GIRLS
SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

**KIAMBATISHO: E.**

**MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi………………….............………………………………(*jina kamili la Mwanafunzi*) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Jina la Mwanafunzi……………………………………………………..

Saini ya mwanafunzi (sio ya kukoroga) ..........................................

Tarehe………………

**Shahidi**

Jina kamili……………………………………………………

Saini…………………………………………………

Tarehe…………………………

KAGERA RIVER GIRLS
SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION

KIAMBATISHO: F.

**A: <u>AHADI YA MZAZI: (ijazwe na mzazi au mlezi wa mwanafunzi)</u>**

Mimi: ___________________________________________ ambaye ni mzazi/mlezi

wa ________________________________________ wa kidato cha _____________

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………

Simu:…………………………………………….

Tarehe:………………

KAGERA RIVER GIRLS SECONDARY SCHOOL
P O BOX 452 - KARAGWE
EDUCATION FOR LIBERATION